

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



**TAARIFA KWA UMMA**

**USITISHAJI WA LESENI ZOTE ZA TAKA HATARISHI AMBAZO HAZIKUFANYIWA  
UHAKIKI NA BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

Kama mnavyofahamu kuwa tarehe 23 Machi 2019 Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira alisitisha biashara ya uingizaji nchini (*importation*) na usafirishaji nje ya nchi (*exportation*) wa taka hatarishi ikiwemo vyuma chakavu, betri zilizotumika na taka za kielektroniki, na kuelekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kufanya uhakiki wa vibali kabla ya kufikia tarehe 02 Aprili, 2019. Kufuatia agizo hilo, Ofisi ya Makamu wa Rais iliwaagiza watu wote wenye leseni za kukusanya taka hatarishi ikiwemo Vyuma Chakavu, Betri zilizotumika na Taka za Kielektroniki kuwa, wapeleke leseni zao halisi (Original Certificates) katika Ofisi za Kanda za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) zilizopo karibu yao kwa ajili ya uhakiki kufikia tarehe 02/04/2019.

Katika zoezi hilo, leseni za makampuni yafuatayo hazikufanyiwa uhakiki:

<b>Na.</b>	<b>JINA KAMPUNI</b>	<b>LA</b>	<b>AINA TAKA HATARISHI</b>	<b>Na. YA LESENI</b>	<b>ANUANI</b>
1	RADS DYNAMICS LTD		Vyuma chakavu	0004	Mtaa wa Kilongwima-Wilaya ya Kinondoni, Kitalu Namba 183 S.L.P 1716 Dar es salaam 0785 551 552
2	GURUKA KWALALA YOUTH GROUP		Vyuma chakavu	0091	S.L.P 21202 DSM 0713 684 086
3	BULYANHULU GOLD MINE (ACACIA)		Kuendesha mtambo wa kurejeleza taka hatarishi	1050	S.L.P 891 Kahama, Shinyanga 28 2520604/0767 200 309
4	S.F.HOZA ENTERPRISES		Mafuta machafu	0600	S.L.P 2052 DSM
5	NGUYA COMPANY LIMITED		Mafuta machafu	1200	S.L.P 768 MWANZA 0765 903 305

6	Nyabigena Mining Cooperative Society Ltd	Mafuta machafu, betri na plastiki zilizotumika	0062	Nyamwaga S.L.P 429, Tarime, Musoma 0717 067 007 <a href="mailto:manager@nyabigenasociety.org">manager@nyabigenasociety.org</a>
7	REDAV EXRAW COMPANY LIMITED	Mafuta machafu	0092	S.L.P 16317 CHALINZE 0717 437 645
8	TANZANIA PETROLEUM SERVICES LTD	Mafuta machafu	2000	Manispaa ya Temeke, DSM 0784 874 329
9	NAGLA GENERAL SHIPPING SERVICES	Mafuta machafu	0098	S.L.P 14011 DSM 0754 316 159
10	CHENG XIN INVESTMENT COMPANY LIMITED	Betri na Plastiki zilizotumika	0093	S.L.P. 76619 DSM 0719 935 250
11	ECHO GENERAL CHEMICAL	Mbolea zenye kemikali	0085	S.L.P 72274 DSM 0713 373 733
12	AFRICAN ASSAY LABORATORIES (T) LTD	Taka za kemikali	0097	S.L.P 1826 MWANZA 0763888086 <a href="mailto:siegmund.laryea@sgs.com">siegmund.laryea@sgs.com</a>

Kwa minajili hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inataarifu umma mambo yafuatayo:-

- i) Leseni zote ambazo hazikuhakikiwa zimefutwa kuanzia tarehe ya taarifa hii.
- ii) Utaratibu wa kupatiwa leseni mpya kwa makampuni yaliyohakikiwa utatangazwa hivi punde.

Mhandisi Joseph Malongo  
**KATIBU MKUU**  
**10 JUNI, 2019**